# SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA YA CHAKULA, DAWA NA VIPODOZI NAMBA 2 YA 2006

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU


VIFUNGU MAELEZO

SEHEMU YA KWANZA
UTANGULIZI

1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Kusomwa.

SEHEMU YA PILI
MAREKEBISHO

3. Marekebisho ya kifungu cha 2.
4. Marekebisho ya kifungu cha 3.
5. Marekebisho ya kifungu cha 4.
6. Marekebisho ya kifungu cha 5.
7. Kuongeza vifungu vipya vya 5A na 5B.
8. Marekebisho ya kifungu cha 6.
9. Marekebisho ya kifungu cha 7.
10. Marekebisho ya kifungu cha 12.
11. Kuongezwa kifungu kipya cha 13A.
12. Kufutwa kwa kifungu cha 14.
13. Kuongezwa kwa vifungu vya 15A, 15B na 15C.
14. Marekebisho ya kifungu cha 20.
15. Marekebisho ya kifungu cha 27.

16. Kuongeza vifungu vya 60A, 60B na 60C.
17. Kuongeza kifungu kipya cha 61A .
18. Kuongezwa kwa kifungu kipya cha 73A.
19. Kuongeza kifungu kipya cha 93A.
20. Kuongeza kifungu kipya cha 119A
21. Marekebisho ya kifungu cha 123.
22. Kuongeza kifungu kipya cha 124A
23. Marekebisho ya Jadweli.

**SHERIA NAMBA 3 YA 2017**

**NIMESAINI**

*Athemi*

**{DR. ALI MOHAMED SHEIN}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

28 Machi ..............................................., **2017**

# SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA YA CHAKULA, DAWA NA VIPODOZI NAMBA 2 YA 2006

---

**IMETUNGWA na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.**

## SEHEMU YA KWANZA
## UTANGULIZI

*Jina fupi na kuanza kutumika.*

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi ya 2017 na itaanza kutumika mara baada ya kutiwa saini na Rais.

*Kusomwa*

**2.** Sheria hii itasomwa pamoja na Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi, Namb. 2 ya 2006 ambayo katika sheria hii itajulikana kama Sheria mama.

## SEHEMU YA PILI
## MAREKEBISHO

*Marekebisho ya kifungu cha 2.*

**3.** Kifungu cha 2 cha Sheria mama kinarekebishwa kama ifuatavyo-

(a) kwa kufuta tafsiri ya neno **"Katibu Mkuu";**

(b) kwa kufuta tafsiri ya neno **"Mrajis"** na kuweka badala yake maneno **"Mkurugenzi Mtendaji"** katika kifungu hiki na pahali popote lilipojitokeza katika Sheria mama;

(c) kwa kufuta tafsiri ya neno **"Bodi"** na kuweka badala yake neno **"Wakala"** katika kifungu hiki na popote lilipojitokeza katika Sheria mama, isipokuwa pale lilipotumika kama Bodi ya Ushauri;

(d) kwa kuongeza tafsiri mpya ya maneno katika mpangilio wa kiherufi kama ifuatavyo-

"biashara ya rejareja ya chakula" maana yake ni uandaaji na ubebaji wa chakula na vifaa vya kuhifadhia katika sehemu ya biashara au sehemu ya mwisho inayotumika kumfikia mlaji na inajumuisha maeneo ya usambazaji, uandaaji, uuzaji, kantini, taasisi inayoandaa chakula, migahawa na sehemu nyengine zinazotumika kwa huduma za biashara ya chakula, madukani, maduka makubwa ya kujihudumia kwa vyakula na vifaa, sehemu za kuuza chakula na biashara ya chakula kwa jumla.

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Ushauri ya Wakala iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 5A cha Sheria hii;

"huduma za afya" maana yake ni utoaji wa huduma za afya au tiba zinazotolewa hospitali, kliniki, vituo vya kuwahudumia wagonjwa na vituo vyote vya utoaji wa huduma za afya kama vile vituo vya huduma ya mama na mtoto na afya ya akili;

"malisho" maana yake ni chembechembe za nafaka au bidhaa, na inajumuisha virutubisho vya nyongeza vilivyotayarishwa au ambavyo havikutayarishwa au vimetayarishwa kwa kiasi kidogo kwa madhumuni ya malisho ya wanyama au samaki;

"Wakala" maana yake ni Wakala wa Kusimamia Chakula, Dawa na Vipodozi ya Zanzibar iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 3 cha Sheria hii;

"Mkurugenzi Mtendaji" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala aliyeteuliwa chini ya masharti ya kifungu cha 6 cha Sheria hii;

"Mwenyekiti" maana yake ni Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 5A(1)(a) cha Sheria hii na inajumuisha mtu mwengine yeyote anayefanya kazi za Mwenyekiti;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"Serikali" maana yake ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Marekebisho ya kifungu cha 3.

**4.** Kifungu cha 3 cha Sheria mama kinafutwa na kuweka badala yake kifungu kipya cha 3 kama ifuatavyo-

Kuazishwa kwa Wakala

**3.**-(1) Kunaanzishwa Wakala wa Serikali itakayojulikana kama Wakala wa Kusimamia Chakula, Dawa na Vipodozi ya Zanzibar kwa kifupi ZFDA.

(2) Wakala itakuwa ni taasisi isiyojitegemea kikamilifu inayoweza kurithiwa na kuwa na muhuri wake, na itakuwa na uwezo wa-

(a) kukopa na kuazima fedha;

(b) kuchukua, kununua au kupata, kumiliki, kubadilisha na kutoa mali inayohamishika na isiyohamishika; na

(c) kufanya au kutekeleza jambo lolote linaloruhusiwa kisheria kufanywa na Wakala.

Marekebisho ya kifungu cha 4.

**5.** Kifungu cha 4 cha Sheria mama kinarekebishwa kama ifuatavyo-

(a) katika kifungu kidogo cha (1)-

(i) kwa kufuta neno "kuweka" katika aya ya (k) na kuweka badala yake neno "kusimamia";

(ii) kufuta aya ya (s) na kuweka badala yake aya ya (s) mpya kama ifuatavyo-

"(s) kudhibiti na kuchukua hatua za kisheria pale itakapoona inafaa, juu ya hatua zisizokubalika za uangamizaji wa bidhaa ambazo zinasimamiwa na Sheria hii;"

(b) kwa kuongeza aya mpya ya (t) kama ifuatavyo-

"(t) kuendesha ukaguzi wa bidhaa zote za tiba zilizopo sokoni kwa ajili ya kuhakikisha usalama na ubora wa bidhaa hizo;"

(c) kufuta kifungu kidogo cha (2) na kuweka badala yake kifungu kipya kama ifuatavyo-

"(2) Wakala, katika utekelezaji wa kazi zake, itakuwa na uwezo wa-

(a) kuendeleza mfumo wa mashauriano na mashirikiano kitaifa na kimataifa na taasisi za umma na binafsi zilizoanzishwa chini ya Sheria yoyote, ambazo zinafanana kazi zake kama zilivyoelezwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki au zinafanya kazi zinazohusiana na chakula, malisho ya wanyama, dawa, vifaa tiba, dawa za mitishamba na vipodozi;

(b) kutambua na kutekeleza viwango kwa mujibu wa vigezo vya kitaifa, kikanda na kimataifa;

(c) kuchukua hatua stahiki kwa ajili ya kuhakikisha ufanisi wa bidhaa kitaifa na kimataifa kwa ajili ya kupambana na kupiga vita usambazaji na utumiaji wa bidhaa zisizofaa na zilizo chini ya viwango vinavyosimamiwa na Sheria hii; na

(d) kukuza mashirikiano kitaifa na kimataifa na kuwianisha kanuni zinazohusiana na bidhaa tiba.

Marekebisho ya kifungu cha 5.

**6.** Kifungu cha 5 cha Sheria mama kinarekebishwa kwa kufuta aya (d) na kuweka badala yake aya mpya kama ifuatavyo-

"(d) kutekeleza kazi yoyote iliyopewa chini ya Sheria hii au sheria nyengine;"

Kuongeza vifungu vipya vya 5A na 5B.

**7.** Sheria mama inarekebishwa kwa kuongeza vifungu vipya vya 5A na 5B mara baada ya kifungu cha 5 kama ifuatavyo-

Kuanzishwa kwa Bodi

**5A.**-(1) Kunaanzishwa Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Kusimamia Chakula na Dawa ya Zanzibar ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais;

(b) Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala;

(c) Mfamasia Mkuu wa Serikali;

(d) Wajumbe wengine watakaoteuliwa na Waziri kutoka:-

(i) Wizara inayohusika na Biashara;

(ii) Wizara inayohusika na Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Mazingira;

(iii) Wakili wa Serikali atakayeidhinishwa na Mwanasheria Mkuu; na

(iv) Jumuiya wa Wafanyabiashara na Viwanda Zanzibar.

(2) Mtu atateuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi endapo atakuwa na elimu na uzowefu usiopungua miaka kumi katika sayansi ya tiba, utawala au fani nyengine yoyote inayohusiana na hizo.

(3) Waziri, kabla hajafanya uteuzi wa wajumbe chini ya kifungu kidogo cha (1) aya (d) ya kifungu hiki, atashauriana na Taasisi husika kwa ajili ya kuhakikisha wajumbe wanakuwa na taaluma inayotosheleza na uzoefu katika fani husika na atazingatia jinsia.

(4) Bodi ya Ushauri itamteua Mwanasheria wa Wakala ili kuwa Katibu wa Bodi.

(5) Masharti yaliyomo katika Jadweli la Sheria hii yatatumika kwa muda wa wajumbe wa Bodi ya Ushauri, kusita

ujumbe, uendeshaji wa vikao na mambo mengine yanayohusiana na Bodi.

Uwezo na wajibu wa Bodi

**5B.**-(1) Bodi itakuwa na uwezo wa kushauri katika utendaji kazi wa Wakala na kipekee itakuwa na uwezo wa-

(a) kushauri utendaji kazi za Wakala zinazohusiana na ukaguzi, usajili, udhibiti wa ubora, mfumo wa ubora wa bidhaa na huduma zinazosimamiwa na Sheria hii;

(b) kutoa miongozo ya kimkakati kwa Wakala katika utekelezaji wa kazi zake;

(c) kushauri juu ya mikakati na mipango ya mwaka na bajeti ya Wakala;

(d) kushauri uendeshaji mzuri, sera, mpango na taratibu zinakuwepo na kutekelezwa;

(e) kuhakikisha matumizi mazuri ya rasilimali, ikijumuisha ushauri katika bajeti ya mwaka ya Wakala;

(f) kupitia utendaji wa Wakala, ukaguzi wa fedha na taarifa nyengine yoyote ya utendaji ya Wakala;

(g) kupendekeza uajiri wa wafanyakazi na mipango ya kuwaendeleza wafanyakazi iliyoandaliwa na uongozi kulingana na rasilimali za Wakala zilizopo kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma; na

(h) kutekeleza jambo lolote kama itakavyoona inafaa kwa ajili ya ufanisi wa utekelezaji wa kazi kwa mujibu wa Sheria hii.

(2) Bodi katika utekelezaji wa kazi zake chini ya Sheria hii, itawajibika kwa Waziri.

Marekebisho ya kifungu cha 6.

**8.** Kifungu cha 6 cha Sheria mama kinafutwa na badala yake kuweka kifungu kipya kama ifuatavyo-

Mkurugenzi Mtendaji

**6.**-(1) Kutakuwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Mtu anaweza kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji ikiwa-

(a) ni Mzanzibari;

(b) ana elimu ya angalau Shahada ya Pili ya Chuo Kikuu kinachotambulika katika fani ya sayansi ya famasia au fani zinazofanana na hizo; na

(c) ana uzoefu wa kazi angalau kwa kipindi cha miaka saba katika fani inayohusika.

(3) Mkurugenzi Mtendaji atakuwa msimamizi mkuu wa Wakala na atakuwa na dhamana ya kuratibu masuala yote ya uongozi na kazi za kila siku za Wakala.

**Marekebisho ya kifungu cha 7.**

**9.** Kifungu cha 7 cha Sheria mama kinafutwa na badala yake kinawekwa kifungu kipya kama ifuatavyo-

**Idara za Wakala**

**7.**-(1) Kunaanzishwa Idara za Wakala kama ifuatavyo:

(a) Idara ya Udhibiti wa Chakula;

(b) Idara ya Dawa, Vipodozi, na Aina nyengine za bidhaa za dawa;

(c) Idara ya Huduma za Maabara, na

(d) Idara ya Huduma za Wakala.

(2) Wakala inaweza kuanzisha idara nyengine au vitengo kama itakavyoona inafaa kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma.

**Marekebisho ya kifungu cha 12.**

**10.** Kifungu cha 12 cha Sheria mama kinafutwa na badala yake kinawekwa kifungu kipya kama ifuatavyo-

**Kamati za wataalamu**

**12.**-(1) Wakala inaweza kuanzisha Kamati za Wataalamu na kuzipa kazi na majukumu ya kutekeleza kwa kila kamati kwa ajili ya kurahisisha utekelezaji wa kazi za Wakala kama itakavyoona inafaa.

(2) Kamati za Wataalamu zilizoanzishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, zinaweza kujiwekea utaratibu wao wa kuendesha vikao.

**Kuongezwa kifungu kipya cha 13A.**

**11.** Sheria mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 13A mara baada ya kifungu cha 13 kama ifuatavyo-

**Uteuzi wa Mchunguzi**

**13A.**-(1) Mkurugenzi Mtendaji atapendekeza kwa Bodi na kutoa tangazo katika Gazeti Rasmi baada ya kuidhinishwa na Bodi, mtu mwenye sifa miongoni mwa wataalamu wa chakula,

dawa, wafamasia, wataalamu wa elimu ya viumbe hai, wataalamu wa teknolojia, wataalamu wa maabara, wahandisi au mwenye taaluma yoyote inayolingana na hizo, kuwa Mchunguzi kwa ajili ya utekelezaji wa masharti ya Sheria hii.

(2) Mtu hatokuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Mchunguzi chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, ikiwa mtu huyo atakuwa na maslahi katika bidhaa za tiba iliyohifadhiwa, inayotengenezwa, inayoingizwa au inayouzwa ambayo inasimamiwa chini ya Sheria hii.

Kufutwa kwa kifungu cha 14.

**12.** Kifungu cha 14 cha Sheria mama kinafutwa.

Kuongezwa kwa vifungu vya 15A, 15B na 15C.

**13.** Sheria mama inarekebishwa kwa kuongeza vifungu vipya vya 15A, 15B na 15C mara baada ya kifungu cha 15 kama ifuatavyo-

Uwazi na ubadilishanaji wa taarifa

**15A.**-(1) Wakala inaanzisha mfumo wa usimamizi kwa kuzingatia mapendekezo ya mashirikiano ya pamoja ya kikanda ili kuleta ubora na uwazi katika utekelezaji wa kazi.

(2) Wakala itaweka mfumo utakaowezesha usimamizi wa utoaji habari ambao utawezesha ubadilishanaji wa habari za usimamizi wa bidhaa.

(3) Wakala itaanzisha mtandao wa kieletroniki utakaowezesha upatikanaji wa nyaraka kama kanuni, sheria, fomu za maombi na usajili wa bidhaa za tiba.

Upatikanaji na udhibiti wa taarifa

**15B.**-(1) Mtu hatoruhusiwa kutoa kwa mtu mwengine au taasisi yoyote taarifa aliyoipata katika utekelezaji wa kazi au wajibu wake chini ya Sheria hii, inayohusiana na kazi au jambo lolote linalomhusu mtu yeyote au kutumia taarifa hiyo kwa manufaa binafsi au kwa faida ya mwajiri wake.

(2) Mtu ataruhusiwa kutoa taarifa-

(a) kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake chini ya Sheria hii, baada ya kupata ruhusa ya maandishi ya Wakala;

(b) endapo atahitajika kutoa taarifa hiyo na Mahakama au kwa mujibu wa sheria; au

(c) ikiwa ni kwa ajili ya maslahi ya umma baada ya kupata ruhusa ya maandishi ya Wakala.

Mfumo wa Kitaifa wa Usimamizi na Tathmini

**15C.**-(1) Wakala itaanzisha Mfumo wa Kitaifa wa Usimamizi na Tathmini utakaohusika na kufanya mapitio na kukadiria Wakala katika utekelezaji wa kazi zake.

(2) Wakala itaandaa taarifa kila baada ya miezi mitatu na kuwasilisha katika Bodi.

Marekebisho ya kifungu cha 20.

**14.** Kifungu cha 20 cha Sheria mama kinarekebishwa kama ifuatavyo:-

(a) katika kifungu kidogo cha (3), kwa kufuta neno "milioni mbili" na badala yake kuweka neno "milioni tatu"; na

(b) katika kifungu kidogo cha (4), kwa kufuta neno "laki moja" na badala yake kuweka neno "laki tatu".

Marekebisho ya kifungu cha 27.

**15.** Kifungu cha 27(2) cha Sheria mama kinarekebishwa kwa kuongeza maneno "biashara ya rejareja ya chakula" katika aya (b) baina ya maneno "kuuza" na "au".

Kuongeza vifungu vya 60A, 60B na 60C.

**16.** Sheria mama inarekebishwa kwa kuongeza vifungu vipya vya 60A, 60B na 60C mara baada ya kifungu cha 60 kama ifuatavyo:-

Ufuatiliaji wa madhara yanayosababishwa na dawa

**60A.**-(1) Wakala itaanzisha programu ya ufuatiliaji wa madhara yanayosababishwa na dawa ili kusimamia na kutoa taarifa kuhusu usalama wa bidhaa za tiba.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, programu hiyo itahusika na-

(a) kusimamia na kuchambua mambo au vitu vinavyoweza kusababisha madhara katika bidhaa zinazosimamiwa chini ya Sheria hii;

(b) kuainisha na kutoa taarifa juu ya vitu vinavyoweza kusababisha madhara wakati wa kufanya majaribio ya matibabu;

(c) kubaini chanzo cha madhara, uchukuaji hatua za fidia kwa waathirika wa madhara ya dawa na uwasilishaji wa taarifa katika mfumo wa usimamizi wa kimataifa; na

(d) hatua za usimamizi zinazofaa pale itakapohitajika, ikijumuisha lakini sio mwisho, katika kufanya mapitio ya vibali vya biashara au masharti ya uwekaji wa alama katika bidhaa za tiba.

(3) Wakala inaweza kutoa miongozo itakayoweka masharti ya lazima ya utoaji wa taarifa na kuwasilisha taarifa za usalama za kila muda za watengenezaji na wasambazaji na utoaji taarifa kwa hiari kwa wataalamu wa utoaji huduma za afya na jamii.

Usimamizi wa ubora

**60B.** Wakala itaanzisha mpango wa kupunguza madhara kwa kupima utakaojumuisha uchukuaji wa sampuli za bidhaa za tiba kupitia mtiririko wa kusambaza, ili kutambua bidhaa ambazo ni za hatari au bidhaa za udanganyifu au zilizo katika kiwango cha chini na kuchukua hatua zinazofaa ili kulinda afya za jamii ikijumuisha utekelezaji wa hatua chini ya Sheria hii.

Kuitisha na kufuta bidhaa za tiba

**60C.** Pale ambapo Mkurugenzi Mtendaji atagundua kuwa bidhaa yoyote ya dawa haipo katika viwango vya utambuzi, kuwa na uwezo, ubora na usafi au haipo katika maelekezo yoyote yaliyoelezwa katika nyaraka za usajili, Mkurugenzi Mtendaji-

(a) ataamuru mtu aliyeruhusiwa kutoendelea na uuzaji wa idadi iliyobaki kwa namna itakavyowezekana; na

(b) ataitisha kiwango cha idadi kilichouzwa.

Kuongeza kifungu kipya cha 61A.

**17.** Sheria mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 61A mara baada ya kifungu cha 61 kama ifuatavyo-

Kuteketeza bidhaa za tiba

**61A**. Kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 61(1) cha Sheria hii, Wakala itaelekeza kwamba bidhaa za tiba ziondelewe katika soko na ziharibiwe kwa mujibu wa masharti ya sheria inayohusika kwa kuzingatia miongozo ya mazingira na namna ambavyo imeelezwa katika kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii.

Kuongezwa kwa kifungu kipya cha 73A.

**18.** Sheria mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 73A mara baada ya kifungu cha 73 kama ifuatavyo-

Kutoa taarifa ya madhara ya dawa hatari

**73A.** Kituo cha afya cha serikali na cha binafsi kitatoa taarifa kwa Wakala kuhusu madhara ya dawa za hatari.

Kuongeza kifungu kipya cha 93A.

**19.** Sheria mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 93A mara baada ya kifungu cha 93 kama ifuatavyo-

Kuwa na alama ya dawa kinyume na sheria

**93A.**-(1) Mtu hatoruhusiwa kumiliki au kuhodhi alama yoyote ya dawa isiyo sahihi.

(2) Mtu yoyote atakayemiliki au kuhodhi alama ya dawa kinyume na masharti ya kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa la jinai na atakapopatikana na hatia atapewa adhabu ya kifungo kisichopungua miezi sita au faini isiyopungua shilingi milioni moja au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Kuongeza kifungu kipya cha 119A.

**20**. Sheria mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 119A mara baada ya kifungu cha 119 kama ifuatavyo-

Tamko na mgongano wa maslahi

**119A.**-(1) Mfanyakazi wa Wakala, mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi au Kamati atatakiwa kutaja maslahi aliyonayo yanayohusiana na bidhaa yoyote ya tiba au jambo lolote ambalo linahitaji kufanyiwa maamuzi.

(2) Tamko la mgongano wa maslahi litashughulikiwa kwa mujibu wa miongozo iliyotangazwa na Waziri kwenye Gazeti Rasmi la Serikali.

Marekebisho ya kifungu cha 123.

**21.** Kifungu cha 123 cha Sheria mama kinarekebishwa kwa kufuta aya (f) na (x).

Kuongeza kifungu kipya cha 124A.

**22.** Sheria mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 124A mara baada ya kifungu cha 124 kama ifuatavyo-

Kumaliza kosa

**124A.**-(1) Mkurugenzi Mtendaji anaweza kukubali kumaliza kosa lililofanywa chini ya Sheria hii au kanuni, kwa kumuagiza mtu huyo kulipa faini iliyowekwa kwa kosa hilo, ikizingatiwa kwamba, endapo mtu aliyefanya kosa-

(a) amekubali kwa maandishi kwamba amefanya kosa na atachukua hatua za uangalifu ili asirudie kosa hilo; na

(b) atalipa faini iliyowekwa na Sheria hii au Kanuni.

(2) Kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, hakutakuwa na mashtaka ya jinai yatakayofunguliwa baadae kwa kosa hilo dhidi ya mtu huyo.

Marekebisho ya Jadweli.

**23.** Jadweli la Sheria mama linarekebishwa kwa kulifuta na kuandikwa upya kama ifuatavyo:-

## JADWELI
## MWENENDO WA VIKAO VYA BODI YA USHAURI
**[Chini ya kifungu cha 5A(5)]**

---

Vikao vya Bodi.

**1.**-(1) Mwenyekiti ataongoza vikao vya Bodi, endapo atakuwa hayupo Makamo Mwenyekiti ataongoza kikao na ikiwa Makamo mwenyekiti naye hayupo, wajumbe watamchagua mjumbe mmoja miongoni mwao kuongoza kikao.

(2) Taarifa pamoja na nyaraka za kikao cha Bodi zitatolewa na kuwasilishwa kwa wajumbe angalau siku saba kabla ya kikao.

(3) Bodi ya Ushauri itakutana kwa kikao cha kawaida angalau mara tatu kwa mwaka katika kuendesha shughuli zake na endapo itatokea dharura, Bodi inaweza kukutana wakati wowote.

(4) Mwenyekiti anaweza kuitisha kikao cha dharura, baada ya kuombwa kwa maandishi na wajumbe wengi, ikizingatiwa kwamba vikao vya dharura havitozidi vikao vitatu.

Makamo Mwenyekiti.

**2.** Bodi itachagua mjumbe mmoja miongoni mwao kuwa Makamo Mwenyekiti.

Maamuzi ya Bodi.

**3.**-(1) Uamuzi wa Bodi utafanywa kwa kura nyingi za wajumbe waliohudhuria na kupiga kura, na endapo itatokea kura kuwa sawa, Mwenyekiti atakuwa na kura ya uamuzi.

(2) Bila ya kujali aya ndogo ya (1) ya aya hii, uamuzi wa Bodi unaweza kufanywa kwa kuwasilisha tamko la maandishi kwa wajumbe na kila mjumbe atatakiwa kueleza mawazo yake kwa maandishi ikizingatiwa kwamba, mjumbe anaweza kuomba uamuzi huo uahirishwe na ujadiliwe na uamuliwe katika kikao.

(3) Tamko la maandishi lililowekwa saini na wajumbe waliopo Zanzibar wasiopungua watano, utakuwa ni uamuzi wa Bodi kama uamuzi huo umefanywa katika kikao.

Akidi ya kikao

**4.** Zaidi ya nusu ya idadi ya wajumbe itakuwa ndio akidi ya kikao cha Bodi.

Uwezo wa Bodi kualika.

**5.** Bodi inaweza wakati wowote katika mkutano wake kumualika mtu yoyote kuhudhuria kama mshauri lakini mtu huyo hataweza kupiga kura katika mkutano huo.

Kumbukumbu za vikao.

**6.** Katibu ataweka na kuhifadhi kumbukumbu za shughuli au vikao vya Bodi, ambazo zitasomwa na kuthibitishwa na Bodi katika kikao kinachofuata kwa kuwekwa saini na Mwenyekiti na Katibu.

Muda wa wajumbe wa Bodi

**7.** Wajumbe wa Bodi ukiacha wajumbe kwa nafasi zao, isipokuwa kama uteuzi wao utasita au utaisha, watashika nafasi hiyo kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia tarehe ya uteuzi na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine kimoja.

Kusita ujumbe

**8.**-(1) Mjumbe wa Bodi atasita kuwa mjumbe ikiwa mjumbe huyo-

(a) atafariki;

(b) atashindwa kutekeleza kazi zake;

(c) atafanya kosa la tabia mbaya au matendo mabaya;

(d) amepatikana na hatia ya kosa la jinai linalohusiana na udanganyifu, kukosa uaminifu au kwenda kinyume na maadili;

(e) ameshindwa kueleza maslahi yake katika jambo lililojadiliwa katika kikao;

(f) ameshindwa kuhudhuria katika vikao vitatu mfululizo bila ya ruhusa ya Mwenyekiti; au

(g) amejiuzulu kwa kutoa taarifa ya maandishi kwa mamlaka ya uteuzi akieleza sababu za kujiuzulu.

(2) Ikiwa Mjumbe wa Bodi, mbali ya wajumbe kwa nafasi zao, atasita kuwa mjumbe kwa sababu yoyote iliyoelezwa chini ya aya ndogo ya (1) ya aya hii, kabla ya kukamilika muda wake, mamlaka ya uteuzi itateua mtu mwengine kushika nafasi hiyo na mtu huyo atashika nafasi hiyo kwa kipindi kilichobaki cha mtangulizi wake.

Maposho ya Bodi

**9.** Wajumbe wa Bodi watalipwa posho kutoka katika fedha za Wakala kwa kiwango kama kitakavyoidhinishwa na Waziri.

Kutangaza mgongano wa maslahi

**10.** Mjumbe ambaye atakuwa na maslahi ya moja kwa moja au vyenginevyo na jambo ambalo litajadiliwa katika kikao cha Bodi, atalazimika kutangaza aina ya maslahi yake kwa Bodi na hatoshiriki katika mjadala wa jambo hilo.

**IMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi Zanzibar tarehe 21 Febuari, 2017.

...................................

RAYA ISSA MSELLEM

***Katibu wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar***